

HALMASHAURI YA WILAYA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

WILAYA YA KONDOA

Fax/Simu 026 2360313

E-Mail: ded@kondoadc.go.tz



Sanduku la Posta 1
KONDOA

Kumb. Na. KDC/L.50/9 VOL.I/27

27/09/2019

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Kwa mujibu wa waraka wa nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha Ajira Mbadala kwa Makatibu Muhtasi chenye Kumb. Na. FA.170/360/01/B/TEMP/36 cha tarehe 21 Juni, 2019 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa alitangaza nafasi za kazi tarehe 26/08/2019 kwa kada za Katibu Mahsusi Daraja la III.

Kutokana na tangazo hili, kutakuwa na usaili wa kada ya Katibu Muhtasi utakaofanyika tarehe 05/10/2019 saa 3.00 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Matokeo ya usaili huo yatabandikwa katika mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na kwenye tovuti ya Halmashauri kwa watakaokuwa wamefaulu.

Wasailiwa wote wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Kufika na vyeti vyao halisi na sio nakala (Vyeti vya kuzaliwa, kidato cha IV na Astashahada).
2. Picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size).
3. Kitambulisho kwa ajili ya utambuzi (cha weza kuwa kitambulisho cha NIDA, Mpiga kura, kitambulisho cha Mkazi au Hati ya kusafiria).
4. Watakaowasilisha "Testimonials", "Provisional of results", "Statement of Results", Hati za matokeo ya Kidato cha IV "Results Slips", hawataruhusiwa kufanya usaili.
5. Muda wa kufika kwenye usaili na tarehe ya usaili kwa wasailiwa wote ni kama ilivyoelekezwa kwenye tangazo hili.

